HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 022 | APRILI - JUNI, 2026

# MAKAMU WA RAIS APOKEA TAARIFA YA MPANGO MKAKATI WA NEMC, ATOA MAELEKEZO YA KUIMARISHA USIMAMIZI WA MAZINGIRA




**Ndani:**

- WAZIRI MKUU AZINDUA MFUMO WA TOCEMS KATIKA KONGAMANO LA MAZINGIRA KUELEKEA NEMC@40
- NEMC YATOA TUZO KWA MSHINDI WA JUMLA WA UTUNZAJI WA MAZINGIRA
- WAZIRI MASAUNI ASITISHA SHUGHULI ZA KIWANDA CHA AFRICAN STEEL KWA UCHAFUZI WA MAZINGIRA

@nemctanzania NemcTVTanzania

NEMC@40 #TunzaMazingiraLindaTaifa

www.nemc.or.tz

# YALIYOMO

1. MAKAMU WA RAIS APOKEA TAARIFA YA MPANGO MKAKATI WA NEMC, ATOA MAELEKEZO YA KUIMARISHA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ....03
2. MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR AWA MGENI RASMI KILELE CHA MAADHIMISHO YA MIAKA 40 YA NEMC ....04
3. WAZIRI MKUU AZINDUA MFUMO WA TOCEMS KATIKA KONGAMANO LA MAZINGIRA KUELEKEA NEMC@40 ....05
4. NEMC YASHIRIKI KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI ....06
5. DKT. NCHIMBI AZURU BANDA LA NEMC MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI ....07
6. FAHAMU NAMNA YA KUHIMILI NA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI ....08
7. NEMC YAMTAMBUA JACKLINE ELIABI MWANAFUNZI WA SHULE YA MSINGI MANYINGA KWA WASILISHO BORA LA UCHUMI MZUNGUKO KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI ....09
8. NEMC NA SWECO YASAINI MKATABA WA UPEMBUZI YAKINIFU-MIRADI YA TAKA KUWA NISHATI ....09
9. NEMC YATOA TUZO KWA MSHINDI WA JUMLA WA UTUNZAJI WA MAZINGIRA ....10
10. NEMC YAKIJANISHA TANZANIA, YAPANDA MICHE YA MITI ELFU AROBAINI NCHI NZIMA ....11
11. KANDA YA MAGHARIBI YAONGEZA KASI YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA ELIMU KWA UMMA ....12
12. NEMC YAKUTANA NA WIZARA YA MAZINGIRA- MAONESHO YA KILIMO KONYA NCHINI UTURUKI ....13
13. WABUNGE WACHARUKA BUNGENI, WATAKA NEMC KUPEWA MENO ....14
14. MIAKA 40 YA NEMC: SAFARI YA TANZANIA KUELEKEA MUSTAKABALI WA KIJANI NA MAENDELEO ENDELEVU ....15
15. DG NEMC AELEZA UMUHIMU WA VYOMBO VYA HABARI KWENYE MASUALA YA MAZINGIRA ....16
16. NEMC NA TORONTO METROPOLITAN UNIVERSITY (TMU) YA NCHINI CANADA ZAKUTANA KUJADILI CHANGAMOTO ZA KIMAZINGIRA ....17
17. NEMC YAUNGANA NA WATANZANIA WOTE KUSHEREHEKEA MEI MOSI ....18
18. BANK YADUNIA YARIDHISHWA NA UTENDAJI WA NEMC ....19
19. MWENYEKITI WA BODI YA NEMC AKIMBIA KILOMITA 5 ....19
20. TAKA SI UCHAFU TENA: TANZANIA YAELEKEA UCHUMI WA KIJANI KUPITIA UREJELEZAJI ....20
21. SERIKALI YASISITIZA UWAJIBIKAJI WA MAZINGIRA KWA VIWANDA NA WADAU WA TAKA HATARISHI ....21
22. NEMC KANDA YA ILALA, HALMASHAURI NA WADAU WA MAZINGIRA WASAFISHA FUKWE ZA DARAJA LA SALENDER ....22
23. NEMC YATAMBUA SHULE BORA ZA UHIFADHI WA MAZINGIRA DAR ES SALAAM ....23
24. WAZIRI MASAUNI ASITISHA SHUGHULI ZA KIWANDA CHA AFRICAN STEEL KWA UCHAFUZI WA MAZINGIRA ....24
25. NEMC YASHIRIKI KONGAMANO LA VIJANA KUJADILI USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA NA DIRA 2050 ....25
26. TAARIFA YA SHUGHULI ZA ROBO MWAKA ZA NEMC KANDA YA MASHARIKI KUSINI (EZS) ....26
27. NEMC KANDA YA ILALA YAENDELEA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA ZUIO LA MIFUKO YA PLASTIKI JNIA ....27

## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria hiyo Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.

**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
Dkt. Menan Jangu

**Mhariri Mkuu:**
Martha P. Kawishe

**Wachangiaji:**
Boniphace Kyaruzi
Tajiri Kihemba
Aziza Muhali
Catherine Ngowi
Alpha Ndahoze
Mary Ntupwa

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# MAKAMU WA RAIS APOKEA TAARIFA YA MPANGO MKAKATI WA NEMC, ATOA MAELEKEZO YA KUIMARISHA USIMAMIZI WA MAZINGIRA




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi (wapili kushoto) akipokea Zawadi ya saa ya ukutani kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhin a Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi (wapili kulia) alipotembelea Ofisi za NEMC jijini Dar es Salaam kuzungumza na watumishi wa taasisi hiyo.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi amepokea taarifa ya Mpango Mkakati wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) alipofanya ziara katika ofisi za Baraza hilo zilizopo Mikocheni, jijini Dar es Salaam, Julai 2, 2026.

Akipokea taarifa hiyo, Makamu wa Rais amepata maelezo kuhusu mwelekeo wa kimkakati wa NEMC katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi ameipongeza NEMC kwa kazi nzuri ya kulinda na kuhifadhi mazingira, hususan katika usimamizi wa Tathmini za Athari kwa Mazingira (EIA) na kuhamasisha matumizi ya nishati safi. Aidha, ameliagiza Baraza kushirikiana na Wizara na taasisi husika kuendeleza mashindano ya usafi wa mazingira katika halmashauri zote nchini, sambamba na utoaji wa zawadi na vyeti kwa washindi ili kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dkt. Richard Stanslaus Muyungi amesema utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 unahitaji kuendelea kuwekeza katika uchumi wa kijani na uchumi wa buluu, sambamba na kuongeza matumizi ya sayansi, teknolojia na tafiti katika kuboresha usimamizi wa mazingira na kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Mhandisi Mwanasha Tumbo amesema maelekezo yaliyotolewa na Makamu wa Rais yameipa NEMC msukumo mpya wa kuendelea kusimamia na kuhifadhi mazingira kwa ufanisi. Aliahidi kuwa Bodi itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwa kuzingatia sheria, sera na vipaumbele vya Serikali ili kuhakikisha mazingira yanaendelea kuhifadhiwa kwa manufaa ya Taifa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Sware Semesi aliwasilisha taarifa ya Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Baraza, akieleza kuwa mpango huo unaweka vipaumbele katika kuimarisha usimamizi wa mazingira, kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma, kuendeleza matumizi ya teknolojia na ubunifu, kuimarisha tafiti za mazingira, pamoja na kukuza ushirikiano na wadau katika kutekeleza agenda ya Taifa ya maendeleo endelevu.

Ziara hiyo imeonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha taasisi zinazosimamia mazingira nchini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, huku ikisisitiza kuwa ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi na wananchi ni msingi muhimu wa kuhakikisha mazingira ya Tanzania yanahifadhiwa na kusimamiwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.



*Baadhi ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wakifuatilia kwa umakini hotuba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi alipotembelea Ofisi ya NEMC Mikocheni jijini Dar es Salaam*

# MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR AWA MGENI RASMI KILELE CHA MAADHIMISHO YA MIAKA 40 YA NEMC






Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla (Katikati), akipokea tuzo ya heshima ilyotolewa na NEMC kwa kinara wa Mazingira nchini ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan siku ya kilele cha NEMC@40. Kushoto ni Waziri wa nchi ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Masauni, na kulia kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, alikuwa Mgeni Rasmi katika kilele cha Maadhimisho ya Miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), yaliyofanyika tarehe 29 Mei, 2026 katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mhe. Hemed alilipongeza Baraza kwa mchango wake mkubwa katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira nchini kwa kipindi cha miaka 40 tangu kuanzishwa kwake. Amesema taasisi hiyo imeendelea kuwa chachu ya utoaji wa elimu ya mazingira, usimamizi wa sheria za mazingira pamoja na kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Aidha, aliwataka Watanzania kuendelea kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa mazingira kwa kuepuka vitendo vinavyosababisha uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Amesisitiza kuwa ushirikiano kati ya Serikali, taasisi, mashirika ya umma na wananchi ni muhimu katika kuhakikisha mazingira yanaendelea kulindwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Akimkaribisha Mgeni Rasmi katika maadhimisho hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Hamad Yusuf Masauni, alisema kuwa NEMC imekuwa nguzo muhimu katika kusimamia na kuratibu shughuli za uhifadhi wa mazingira nchini kwa kipindi cha miongo minne. Alibainisha kuwa mafanikio yaliyopatikana katika usimamizi wa mazingira yametokana na ushirikiano mzuri kati ya Serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi.

Mhe. Masauni aliongeza kuwa katika kipindi chote cha miaka 40, NEMC imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ubunifu, hatua iliyochangia kuimarika kwa utekelezaji wa sheria za mazingira, kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya mazingira pamoja na kuimarisha usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuhakikisha inazingatia misingi ya uhifadhi wa mazingira.

Katika maadhimisho hayo, Mhe. Hemed pia alisisitiza umuhimu wa kuimarisha matumizi ya teknolojia na ubunifu katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Alieleza kuwa matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, pamoja na uwekezaji katika nishati safi na usimamizi bora wa taka, yatachangia kwa kiasi kikubwa katika kulinda rasilimali za asili na kuimarisha ustawi wa jamii.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alieleza kuwa katika kipindi cha miaka 40 ya uwepo wake, Baraza limefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kuimarisha utekelezaji wa sheria za mazingira, kufanya tathmini za athari kwa mazingira za miradi ya maendeleo na kuendesha kampeni za uelimishaji kwa umma. Maadhimisho hayo yalitoa fursa ya kutathmini mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo na kuweka mikakati madhubuti ya kuendeleza uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira nchini.

Maadhimisho ya miaka 40 ya NEMC yaliwakutanisha viongozi wa Serikali, wadau wa mazingira, taasisi za umma na binafsi, washirika wa maendeleo pamoja na wananchi kwa lengo la kuadhimisha mafanikio ya taasisi hiyo na kujadili mustakabali wa usimamizi wa mazingira nchini katika kukabiliana na changamoto za sasa na baadae.

# WAZIRI MKUU AZINDUA MFUMO WA TOCEMS KATIKA KONGAMANO LA MAZINGIRA KUELEKEA NEMC@40

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alizindua mfumo wa kidigitali wa kufuatilia Uchafuzi wa Mazingira (TOCEMS) wakati wa Kongamano la Kisayansi lililofanyika ukumbi wa JNICC siku chache kabla ya kilele cha maadhimisho ya Miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Katika kongamano hilo, Dkt. Nchemba amelipongeza Baraza kwa juhudi kubwa na mafanikio ya miongo minne katika Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Katikati), akibonyeza kompyuta mpakato kama Ishara ya uzinduzi wa mfumo wa TOCEMS siku ya Kongamano la Mazingira lililofanyika tarehe 28 Mei, katika ukumbi wa JNICC Jijini Dar es salaam, kulia kwake ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni na kushoto kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi*

Kongamano hilo lililobeba kaulimbiu "NEMC@40: Tunza Mazingira, Linda Taifa." Lilikuwa na lengo la kujadili mchango wa usimamizi wa mazingira katika maendeleo endelevu ya Taifa pamoja na kutafuta suluhisho la changamoto mbalimbali za kimazingira zinazoikabili nchi.

Akizungumza na washiriki, Dkt. Nchemba alisisitiza kuwa Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na NEMC ili kuhakikisha Sheria, Kanuni na miongozo ya mazingira inatekelezwa ipasavyo katika sekta zote za maendeleo. Alibainisha kuwa uhifadhi wa mazingira si jukumu la taasisi moja pekee, bali ni wajibu wa kila mwananchi na kila sekta kwa mustakabali wa Taifa na vizazi vya baadae. Aidha, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kudhibiti shughuli zinazosababisha uharibifu wa mazingira.

Mfumo wa TOCEMS uliozinduliwa ulilenga kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli zinazoweza kusababisha uchafuzi wa mazingira nchini. Dkt. Nchemba alieleza kuwa mfumo huo utaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa taarifa, ufuatiliaji wa viashiria vya uchafuzi na kurahisisha utoaji wa taarifa kwa mamlaka husika ili kuchukua hatua za haraka. Hatua hiyo inatarajiwa kuboresha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa mazingira.




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Katikati) akiwa katika picha ya Pamoja na baadhi ya watumishi wa NEMC mara baada ya ufunguzi wa Kongamano la Mazingira tarehe 28, Mei, 2026 ukumbi wa JNICC Jijini Dar es salaam. Kulia kwake ni Waziri wa Nchi ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhandisi Yusuph Masauni, na Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi.*

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, aliahidi kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na wadau kuhakikisha rasilimali za Taifa zinalindwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, alisema katika miaka 40 Baraza limefanikiwa kuimarisha usimamizi kupitia tafiti, elimu kwa umma, tathmini za athari za mazingira na ukaguzi wa miradi. Mafanikio hayo, alisema, yametokana na ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na wadau kutoka Serikali, sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za elimu na wananchi, wote wakijadili matumizi ya teknolojia na mikakati ya kuimarisha usimamizi wa mazingira. Kongamano lilikuwa sehemu ya maandalizi ya kilele cha maadhimisho ya miaka 40 ya NEMC yaliyofanyika Mei 29, 2026. NEMC iliahidi kuendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia, tafiti na kampeni za elimu ili kuhakikisha Tanzania inabaki na mazingira salama na endelevu kwa vizazi vijavyo.

# NEMC YASHIRIKI KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilishiriki kilele cha Maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika tarehe 5 Juni 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete (JKCC) Jijini Dodoma yaliyobeba kaulimbiu isemayo Dira 2050- Tushirikiane kukijanisha Tanzania

Mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Emmanuel Nchimbi ambapo pamoja na mambo mengine alizindua mkakati wa Kitaifa wa kukijanisha Tanzania.

Pamoja na mambo mengine Makamu wa Rais Mhe. Dkt Nchimbi alitoa maagizo kumi kwa Serikali na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

1. Mamlaka za Serikali za mitaa hususani manispaa na majiji kuanzisha Bustani za kijani na kuhakikisha zinatunzwa ipasavyo
2. Mamlaka zinazotoa vibali vya ujenzi kuweka sharti na kusimamia ili kila kibali cha ujenzi kinachotolewa kiambatane na agizo la kupanda miti isiyopungua mitano (5)
3. Wakala wa huduma za misitu Tanzania kuhakikisha uwepo wa miche ya kutosha ili kurahisisha na kuwezesha zoezi la upandaji wa miti nchini
4. Sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa na wakala wa huduma za misitu kuimarisha udhibiti wa uharibifu wa maeneo yote yanayopandwa miti
5. Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia kituo chaTaifa cha kuratibu Kaboni kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kubainisha misitu inayofaa na kuisajili katika biashara ya Kaboni
6. Wizara za kisekta kujumuisha fursa za biashara ya Kaboni katika mipango, program na Miradi yao hususani fursa zinazoendana na Sekta husika
7. Wizara ya Ardhi isimamie utekelezaji na uzingatiaji wa mipango miji ya matumizi ya ardhi ili kupunguza au kuondoa kabisa changamoto za uharibifu wa mazingira zinazotokana na matumizi ya ardhi yasiyo endelevu
8. Mamlaka za Serikali za mitaa kupitia kifungu cha 89 cha Sheria ya Serikali za mitaa Mamlaka ya miji sura ya 288 kuimarisha mifumo ya usimamizi wa taka hususani kuanzia vituo vya kuchakata taka ili kupunguza kiasi cha taka katika madampo na kuchangia urejelezaji
9. Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na utalii na Wizara yam aji kuimarisha usimamizi endelevu wa maeneo ya ardhi oevu
10. Taasisi za utafiti kufanya tafiti kuhusu mimea, viumbe vamizi ambavyo vinazidi kuongezeka na kuathiri mifugo na mimea mingine katika maeneo mbalimbali nchini

Aidha Mheshimiwa Makamu wa Rais alitoa wito kwa umma juu ya suala la ulinzi na uhifadhi wa mazingira. Alisema,

”Suala la ulinzi na usimamizi wa mazingira halina mbadala, kwakuwa mazingira yetu ndio uhai wetu, wito wangu kwa kila mmoja wetu ni kuwajibika, kuhakikisha kwamba suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira hususani udhibiti wa taka linapewa kipaombele, kwa kufanya hivyo tutaweza kulinda mazingira yetu na kupunguza Athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi. Kwa niaba ya Mhe. Rais napenda kutoa shukrani na pongezi kwa wadau wote wa mazingira hususani mashirika ya umoja wa mataifa, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, sekta binafsi, vyombo vya Habari na wananchi wote kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira kwa ujumla”

Maadhimisho hayo pia yalitanguliwa na Maonesho ya wiki nzima yenye kutoka elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa wadau ambapo NEMC kama mdau wa Mazingira alitekeleza Dira hiyo kwa vitendo.



*Baadhi ya watumishi wa NEMC wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi wakiwa kwenye banda la maonesho la NEMC kwenye Maonesho ya Wiki ya Mazingira 2026 jijini Dodoma*

# DKT. NCHIMBI AZURU BANDA LA NEMC MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt Emmanuel Nchimbi akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Kanda ya Kati Bw. Novatus Mushi, alipotembelea Banda la NEMC kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 5 katika viwanja vya Jakaya Kikwete (JKCC) Jijini Dodoma.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Emmanuel Nchimbi, alitembelea banda la Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) siku ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, yanayoadhimishwa tarehe 5 Juni ya kila mwaka. Ziara hiyo ilimpa fursa ya kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na NEMC katika kusimamia, kulinda na kuhifadhi mazingira nchini kwa lengo la kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Akiwa katika banda hilo, Mhe. Dkt. Nchimbi alipatiwa maelezo kuhusu majukumu ya NEMC, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa sheria za mazingira, pamoja na mikakati mbalimbali inayotekelezwa na Baraza katika kukabiliana na changamoto za uchafuzi wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi. Pia alipata fursa ya kuona vifaa, machapisho na teknolojia zinazotumika katika utoaji wa elimu ya mazingira na usimamizi wa shughuli za maendeleo zinazoweza kuwa na athari kwa mazingira.

Maadhimisho ya mwaka huu yalifanyika chini ya kaulimbiu isemayo, "Dira 2050: Tuwajibike Kukijanisha Tanzania," ambayo ililenga kuhamasisha ushiriki wa wananchi, taasisi za umma na binafsi pamoja na wadau wa maendeleo katika kuhifadhi mazingira, kupambana na uharibifu wa mazingira na kuendeleza matumizi endelevu ya rasilimali asilia kwa maendeleo ya Taifa.

Kupitia maadhimisho hayo, wananchi walipata fursa ya kujifunza kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, upandaji miti, usimamizi bora wa taka, pamoja na hatua mbalimbali zinazoweza kuchukuliwa katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. NEMC iliendelea kutumia maadhimisho hayo kama jukwaa la kutoa elimu na kuhamasisha jamii kuhusu wajibu wa kila mmoja katika kulinda mazingira kwa ajili ya ustawi wa Taifa na vizazi vijavyo.

# FAHAMU NAMNA YA KUHIMILI NA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI



*na Mha. Dkt. Befrina Igulu*

Mabadiliko ya tabia nchi yananguzo mbili muhimu ambazo ni "Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi" yaani Climate change Mitigation na "Kuhimili mabadiliko ya tabia nchi" yaani Climate change adaptation. Hizi ni aina mbili za mikakati tofauti ambazo mustakabali maisha ya vizazi zijavyo, shughuli za maendeleo na mifumo ya ikolojia inategemea jamii ya sasa kuweza kufanikisha mikakati hii kwa usahihi na ufanisi.

Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kunalenga kudhibiti chanzo cha visababishi vya mabadiliko ya tabia nchi. Hii inamaanisha kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na hasa kubadilisha mifumo inayozalisha hewa ukaa. Mathalani; nishati mbadala na safi inaweza kutumika badala ya nishati za mafuta ya jamii za petroli katika vyombo vya usafiri na viwanda. Majengo kuwa na mifumo ya matumizi madogo ya umeme na nishati. Ni jambo la msingi kukumbuka kuwa kila tani ya uzalishaji hewa ukaa unayoepuka husaidia kupunguza ongezeko la joto duniani na kupunguza kiwango cha athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Kuhimili mabadiliko ya tabia nchi kunalenga namna ya kujenga ustahimilivu katika jamii, shughuli za maendeleo na mifumo ya ikolojia ili kuishi na athari zilizopo kwa sasa na tarajiwa zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi. Jambo muhimu la kukumbuka ni kuwa pamoja na hatua zinazochukuliwa kupunguza hewa ukaa bado kuna athari zinazojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kama vile mafuriko, dhoruba, ukame na mengineyo. Yote haya yanaongezeka kwa kasi na kiwango kikubwa. Kuhimili mabadiliko ya tabia nchi inamaanisha kuandaa jamii na shughuli za maendeleo kwa: kukabili mafuriko, kuwa na mifumo ya vizuizi vya asili, mazao yanayostahimili ukame, mifumo ya tahadhari mapema, miji yenye miundombinu inayostahimili athari za mabadiliko ya tabia nchi. Na hili linalengo kubwa la kulinda maisha, shughuli za jamii, na mifumo ikolojia kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yasiyoepukika.

Mihimili hii miwili inatupa ufahamu muhimu wa kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi wakati huo huo tunaendanaje na kile ambacho tumeshaa kisababisha. Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi bila kuwa na uhimilivu wa athari za madabailiko ya tabia nchi huacha jamii bila kinga. Na uhimilivu wa athari za tabia nchi bila kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ni kuacha athari za mabadiliko ya tabia nchi yazidi kushamiri na kuelemea mifumo ya uhimilivu iliyowekwa na kuleta madhara zaidi.

Hii ndio sababu kubwa inayopelekea Serikali itilie mkazo kwa shughuli za maendeleo na ujenzi wa miji kuzingatia zana zote mbili. Hatua za mabadiliko ya tabianchi si sera ya mazingira tu ni usimamizi wa athari, uvumbuzi wa teknolojia za mbadala wa vitu, na uongezaji wa thamani katika bidhaa zinazozalishwa kama taka. Hatua ambazo Tanzania imeshachukua hadi sasa ni pamoja na matumizi ya nishati safi za kupikia zenye lengo la kupunguza matumizi ya kuni na pia kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa; ukusanyaji sanifu wa taka na matumizi ya taka katika kutengeneza samadi, vyakula vya mifugo na kutumika katika uzalishaji wa nishati; ulinzi wa vyanzo vya maji kwa kupunguza shughuli za jamii kama kilimo, makazi na ukataji miti katika kingo za vyanzo vya maji, hii ikilenga kuacha ukingo wa mto kukabiliana na mafuriko, kuhama njia na kuathiri jamii zililokaribu na bila kusahau vyanzo kuendelea kutoa maji ambayo yanahitajika kwa jamii na ikolojia; matumizi ya magari ya mwendokasi na treni za umeme zinazolenga kupunguza idadi kubwa ya vyombo vya usafiri ambavyo vinatumika na kuchangia uzalishaji wa hewa ukaa.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linajukumu kubwa la kitaifa katika kuhakikisha dhana hizi mbili zinaingizwa katika shughuli za maendeleo ili kuwezesha jamii kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza athari zake nchini Tanzania. Hili linafanyika kwa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, kuingiza masuala ya tabianchi katika Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA), na kuhakikisha ufuatiliaji na utekelezaji wa masharti ya miradi kupitia ukaguzi na hatua za kisheria. Hii ni pamoja na kuhakikisha miradi yote ya kimaendeleo na shughuli za jamii zinakuwa na mifumo stahiki ya kupunguza uzalisha wa hewa ukaa na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ili kuwe na maendeleo endelevu. Baraza pia ni chombo kilichoidhinishwa na Mfuko wa Kuhimili (Adaptation Fund), inahamasisha rasilimali kwa ajili ya miradi ya kustahimili mabadiliko ya tabianchi katika sekta mbalimbali. Hii inasaidia kuwezesha Baraza kuweza kuwa na miradi ya uhimilivu unayosadia jamii ambazo zimesha athirika zaidi na mabadiliko ya Tabia Nchi. Kwa njia hii, NEMC ni msimamizi na pia mhamasishaji wa ubunifu, kuhakikisha maendeleo ya Tanzania yanabaki endelevu na yenye ustahimilivu dhidi ya changamoto za tabianchi.

Wito wa Baraza kama chombo kikuu cha mazingira ni punguza uzalishaji wa hewa ukaa kadri iwezekanavyo na kwa haraka, na kujenge ustahimilivu katika jamii. Kadiri hatua zinavyoongezeka mapema, ndivyo kizazi kijacho kitakavyokuwa na chaguo nyingi zaidi.

# NEMC YAMTAMBUA JACKLINE ELIABI MWANAFUNZI WA SHULE YA MSINGI MANYINGA KWA WASILISHO BORA LA UCHUMI MZUNGUKO KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilimtambua mwanafunzi wa Darasa la Sita, Jackline Eliabi wa Shule ya Msingi Manyinga, Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro, kwa uwasilishaji wake bora wa dhana ya Uchumi Mzunguko katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akimkabidhi zawadi mwanafunzi wa Shule ya msingi Manyinga, Jackline Eliabi kwa wasilisho bora la uchumi mzunguko katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Juni 5 katika viwanja vya Jakaya Kikwete (JKCC) Jijini Dodoma*

Jackline alipata pongezi na kutunukiwa zawadi baada ya kuwasilisha kwa umahiri dhana hiyo muhimu inayohamasisha matumizi endelevu ya rasilimali, upunguzaji wa taka na uhifadhi wa mazingira. Uwasilishaji wake ulionesha uelewa mkubwa wa masuala ya mazingira na mchango wa wanafunzi katika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira kwa maendeleo endelevu.

Zawadi hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, ikiwa ni kutambua mchango wa wanafunzi katika kusukuma gurudumu la uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Dkt. Semesi alieleza kuwa wanafunzi ni wadau muhimu katika juhudi za kulinda mazingira na kwamba wao ndio mabalozi wa baadaye wa mazingira watakaosaidia kuendeleza agenda ya maendeleo endelevu kwa manufaa ya Taifa na vizazi vijavyo.

# NEMC NA SWECO YASAINI MKATABA WA UPEMBUZI YAKINIFU-MIRADI YA TAKA KUWA NISHATI

NEMC kwa kushirikiana na Kampuni ya SWECO AB ya Sweden, walisaini mkataba wa kufanya upembuzi yakinifu kwa mradi wa kubadili taka kuwa nishati tarehe 16 Aprili 2026 katika ofisi za NEMC, jijini Dar es Salaam.

Upembuzi huo yakinifu utatekelezwa katika Mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza na unafadhiliwa na Shirika la maendeleo la Swedfund AB kutoka Sweden.

Lengo la mradi huu ni kuchochea ukuaji wa uchumi rejelezi na kufanya taka kuwa fursa, hususan taka ozo, kwa kuzigeuza kuwa rasilimali yenye kuweza kutumika kwa ajili ya kuzalisha umeme au kuzalisha mafuta ya kuendesha mitambo mbalimbali ikiwemo magari katika maeneo ya mijini.

Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza katika kukabiliana na changamoto ya ongezeko la taka zinazozalishwa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.



*Pichani ni Mkurugenzi wa Idara ya Tafiti za Mazingira (NEMC), Dkt. Menan Jangu akisaini mkataba wa Mashirikiano.*

Kupitia mradi huu, NEMC inaendelea kusisitiza usimamizi endelevu wa taka, utenganishi wa taka katika vyanzo na matumizi bora ya rasilimali kwa ajili ya kulinda mazingira na kuchochea maendeleo ya uchumi wa kijani.

# NEMC YATOA TUZO KWA MSHINDI WA JUMLA WA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilikabidhi tuzo kwa Mkoa wa Njombe ikiwa ni Mshindi wa Jumla wa Shindano la Afya na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka 2024.

Tuzo hiyo ilikabidhiwa na Mgeni Rasmi wa Mkutano Maalum wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa ambaye ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba Aprili 22, 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Arusha (AICC).

Akimkabidhi Tuzo hiyo Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mhe. Profesa Riziki Silas Shemdoe alisema tuzo hiyo imetolewa na NEMC kwa kuthamini mchango wa Mkoa wa Njombe katika Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Akizungumza na baadhi ya Waheshimiwa Wenyeviti na Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Njombe mara baada ya zoezi hilo la utoaji wa Tuzo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi aliwapongeza kwa kuchukulia suala la Mazingira kwa umuhimu mkubwa na kutoa rai kwa Halmashauri nyingine Nchi nzima kuiga mfano wa Mkoa wa Njombe.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba akikabidhi tuzo ya heshima kwa Mkoa wa Njombe ikiwa ni Mshindi wa Jumla wa Shindano la Afya na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka 2024. Tuzo hiyo ilitolewa na Baraza la Taifa la Hifadhina Usimamizi wa Mazingira (NEMC0*

Akitoa neno la Shukrani kwa niaba ya Mkoa wa Njombe, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Makete, Mhe. Rabson A. Mahenge aliiishukuru NEMC kwa kuthamini mchango wao katika kutunza mazingira na alisisitiza kuwa NEMC iendelee kutoa maelekezo kwani Mkoa wa Njombe utatekeleza na matokeo yataonekana.

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo NEMC huendesha mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira kila mwaka. Mwaka 2024, na miaka mingine Mkoa wa Njombe umekuwa kinara katika uimarishaji wa huduma za usafi wa Mazingira.

Mkoa huo umekuwa ukiongoza kwa kuwa na kaya zenye vyoo bora, usafi wa mazingira na usafi binafsi katika ngazi ya kaya, Shule na Vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Mkoa umekuwa mfano na darasa la kujifunza kwa Halmashauri nyingine katika masuala ya udhibiti wa taka ngumu na maji taka. Hali hii ya Mkoa ilichangiwa na viongozi ngazi zote kuamua pamoja na wananchi kuyapa kipaumbele masuala ya usafi wa mazingira, hali iliyochangia Mkoa kutopata visa vya ugonjwa wa kipindipundu kwa muda mrefu na wananchi kuendelea kujishughulisha na shughuli za kiuchumi.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi (Katikati) akifurahia tuzo waliyoitoa kwa Mkoa uliokuwa kinara wa Mazingira (Njombe) pamoja na Maafisa wa Baraza mara baada ya zoezi la kutunuku tuzo hiyo kukamilika.*

# NEMC YAKIJANISHA TANZANIA, YAPANDA MICHE YA MITI ELFU AROBAINI NCHI NZIMA



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt Immaculate Sware Semesi akiwa na baadhi ya Menejimenti ya NEMC wakipanda mti katika eneo la Kituo kinachojengwa Cha kudhibiti matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu-Geita*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Halmashauri za Miji, Halmashauri za Wilaya, Shule za msingi, wadau wa mazingira pamoja na Mabalozi wa Mazingira, lilipanda miche ya miti elfu arobaini katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni sehemu ya kuelekea maadhimisho ya miaka 40 tangu kuanzishwa kwa Baraza hilo.

Zoezi hilo lilifanyika kupitia kanda 13 za NEMC nchi nzima huku likiambatana na utoaji wa elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa mazingira kwa wananchi, wanafunzi na wadau kwa lengo la kuongeza uelewa wa umuhimu wa utunzaji wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza katika zoezi hilo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi alisema Baraza hilo limekasimiwa wajibu na dhamana ya kuhifadhi na kusimamia mazingira kwa mujibu wa Sheria, hivyo lina wajibu wa kuhakikisha mazingira yanaendelea kulindwa kwa manufaa ya Taifa na vizazi vijavyo.

Dkt. Semesi alisema maadhimisho ya miaka 40 ya NEMC yalilenga kuonesha mafanikio na dhamira ya Baraza hilo katika kusimamia mazingira kwa vitendo kupitia kampeni ya upandaji miti na utoaji wa elimu kwa jamii.

“Tunapoelekea maadhimisho ya miaka 40 tangu kuanzishwa kwa NEMC tunataka kuadhimisha kwa vitendo. Lengo letu ni kuiona Tanzania ya kijani na yenye hewa safi,” alisema Dkt. Semesi.

Aidha alisema kampeni hiyo pia ililenga kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameendelea kusisitiza umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za asili nchini.

Kanda za NEMC zilizoshiriki katika zoezi hilo ni pamoja na Kanda ya Kati Dodoma, Kanda ya Kaskazini Arusha, Kanda ya Bagamoyo, Kanda ya Kusini Mtwara, Kanda ya Ziwa Victoria Magharibi Geita, Kanda ya Ziwa Victoria Mashariki Mwanza, Kanda ya Temeke, Kanda ya Ilala, Kanda ya Mashariki Kaskazini, Kanda ya Mashariki Kusini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Magharibi Kigoma pamoja na Kanda ya Morogoro Rufiji, huku NEMC ikieleza kuwa zoezi hilo ni endelevu kwa maendeleo ya mazingira nchini

# KANDA YA MAGHARIBI YAONGEZA KASI YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA ELIMU KWA UMMA



*Baadhi ya watumishi wa NEMC Kanda ya Magharibi wakifanya usafi katika eneo la soko la Nazareth Kigoma mjini.*

Katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2025/2026, Kanda ya Magharibi imeendelea kuonesha mafanikio makubwa katika usimamizi wa mazingira kupitia utekelezaji wa majukumu ya kisheria na kuelimisha yaliyolenga kuimarisha uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora.

Kanda hiyo ilifanya ukaguzi katika miradi 50 ya maendeleo iliyojumuisha viwanda, migodi, vituo vya mafuta, hoteli, kumbi za starehe, maghala ya kemikali na hatarishi, masoko pamoja na madampo. Ukaguzi huo uliendelea kuimarisha uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuongeza ubora wa hifadhi ya mazingira katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa miradi.

Sambamba na hilo, Kanda ya Magharibi iliendelea kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa kusajili jumla ya miradi 24 ya maendeleo kwa ajili ya kufanyiwa tathmini hiyo. Aidha, miradi 9 ilikamilisha taratibu zote zinazohitajika na kuidhinishwa kupatiwa vyeti vya mazingira, hatua inayodhihirisha kuongezeka kwa mwitikio wa wawekezaji na wadau wa maendeleo katika kuzingatia matakwa ya sheria za mazingira.

Katika jitihada za kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira, kanda hiyo ilitumia vyombo vya habari kufikisha elimu kwa umma. Jumla ya vipindi 10 vya redio vilirushwa kupitia redio za jamii na taifa, huku vipindi 3 vya televisheni na makala maalumu 1 vikitoa ujumbe wa kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika uhifadhi wa mazingira.

Miongoni mwa matukio muhimu yaliyotawala kipindi hicho ni maadhimisho ya miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), ambapo Kanda ya Magharibi ilishiriki katika shughuli za usafi wa mazingira, upandaji miti na utoaji wa elimu kwa wananchi. Katika maadhimisho hayo, jumla ya miti 3,000 ilipandwa ambapo Mkoa wa Kigoma miti 1,900, Katavi miti 700 na Tabora miti 400. Miti hiyo ilipandwa katika shule, vyuo na vituo vya kutolea huduma za afya ili kuchangia juhudi za kukijanisha Tanzania na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kanda hiyo pia ilishiriki kikamilifu katika Maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani ya mwaka 2026 yaliyobeba kaulimbiu isemayo, "Dira 2050: Tuwajibike Kukijanisha Tanzania." Kupitia maadhimisho hayo, wananchi walipata elimu kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira na wajibu wao katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Kilele cha maadhimisho hayo kwa upande wa Kanda ya Magharibi kilifanyika katika Kijiji cha Mpeta, Wilaya ya Uvinza, Mkoa wa Kigoma. Shughuli mbalimbali zikiwemo usafi wa mazingira katika Soko la Mpeta na upandaji miti katika Shule ya Msingi Mpeta zilifanyika kwa ushirikiano wa wananchi na wadau mbalimbali wa mazingira. Mgeni rasmi katika tukio hilo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mhe. Dinnah Mathaman.

Mafanikio haya yaliendelea kuonesha dhamira ya Kanda ya Magharibi katika kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho, huku ikiendelea kutoa elimu na kusimamia utekelezaji wa sheria za mazingira katika maeneo yote ya kanda hiyo.

# NEMC YAKUTANA NA WIZARA YA MAZINGIRA- MAONESHO YA KILIMO KONYA NCHINI UTURUKI

Yabadilishana uzoefu katika masuala mazima ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilikutana na kufanya mazungumzo na Wizara ya Mazingira, Maendeleo ya Miji na Mabadiliko ya Tabianchi, Taasisi ya Utafiti wa Udongo, Maji na Majanga, Idara ya Maji safi na Maji Taka, Taasisi ya Mradi wa Maendeleo ya Mji wa Konya na Kampuni ya Turko wakati wa maonesho ya zana bora na pembejeo za kilimo na kilimo hifadhi katika Mji wa Konya nchini Uturuki

Mazungumzo hayo yalilenga kubadilishana uzoefu katika masuala ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa na kujifunza mbinu bora zinazotumika katika kukabiliana na changamoto za kimazingira.

Akifafanua utekelezaji wa majukumu kutoka NEMC, wakati wa mazungumzo hayo Afisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi Bi Suzan Chawe alisema wajibu wa Baraza ni kushauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu masuala ya Mazingira na kusimamia Uhifadhi wa Mazingira kwa mujibu wa Sheria na kuainisha majukumu mengine ya Baraza iliyonayo kuwa ni kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii, Utafiti wa Mazingira, Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria na kutoa elimu ya Mazingira.

Mada zilizojadiliwa ni pamoja na matumizi ya zana zenye kuzingatia kilimo hifadhi, utafiti na utoaji taarifa za kimazingira kwa umma, ushirikishaji wa wadau katika utekelezaji wa Sheria za mazingira, utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii hususani mashuleni, pamoja na mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, wataalam wa Mazingira kutoka Konya walisisitiza umuhimu wa tafiti za kisayansi katika sekta mbalimbali ili kuboresha maamuzi ya kikanuni na kisheria na namna ya kudhibiti uchafuzi unaotokana na shughuli za viwanda.

Mbali na mazungumzo hayo, NEMC pia ilipata fursa ya kutembelea maonesho ya kilimo nchini humo yaliyolenga kuonesha zana zenye kukuza kilimo hifahi, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuhamasisha Maendeleo endelevu yenye kuzingatia usimamizi bora wa mazingira kwa kizazi kijacho.

Ujumbe wa NEMC kutoka Tanzania, ulioambatana na wawakilishi kutoka Wizara ya Kilimo pamoja na wadau wa mazingira, pia ulipokelewa na Balozi wa Tanzania nchini Uturuki Mhe. Iddi Seif Bakari hatua iliyoonesha dhamira ya nchi katika kuimarisha diplomasia ya mazingira na ushirikiano wa kimataifa

Faida za ujio wa NEMC kwenye maonesho hayo pamoja na mazungumzo yaliyofanyika yanatarajia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya NEMC pamoja na kuimarisha mahusiano kati ya Tanzania na Uturuki katika sekta ya mazingira.

*Kaimu Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma (NEMC) Bi. Martha Kawishe akichagia jambo wakati wa majadilino mara walipozuru Wizara ya Mazingira, maendeleo ya miji na Mabadiliko ya Tabianchi -Konya nchini Uturuki. Kulia Kwake ni Afisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi (NEMC) Bi Suzan Chawe.*



# WABUNGE WACHARUKA BUNGENI, WATAKA NEMC KUPEWA MENO



*Mbunge wa Katavi, Mhe. Thomas Kampala akichangia mada katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ya Kuifanya NEMC kuwa Mamlaka kamili ili iweze kusimamia sheria ya Mazingira kwa ukamilifu, katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma.*

Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliibuka na hoja nzito wakichangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), wakitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupewa mamlaka kamili pamoja na rasilimali za kutosha ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Wakichangia kwa nyakati tofauti baada ya hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mhandisi Hamad Y. Masauni, wabunge hao walisema licha ya NEMC kupewa jukumu la kusimamia na kulinda mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), bado haina nguvu ya kisheria ya kutosha kuchukua hatua kali dhidi ya waharibifu wa mazingira.

Akichangia mada hiyo, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Tabora, Mhe. Christina Mndeme, alimpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha NEMC kupata maabara inayotembea, akisema hatua hiyo itaongeza ufanisi katika udhibiti wa mazingira kwa kutumia ushahidi wa kisayansi. Aidha, alisisitiza kuwa endapo NEMC itapewa mamlaka kamili, uwajibikaji utaongezeka, ufanisi utaimarika na taasisi hiyo itakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kisheria bila muingiliano wowote kutoka taasisi nyingine.

Naye Mbunge wa Katavi, Mhe. Thomas Kampala, alipoongea alisisitiza kuwa ipo haja ya haraka ya kuipa NEMC "meno" ili iweze kuchukua hatua stahiki dhidi ya vitendo vya uharibifu wa mazingira vinavyoongezeka nchini. Alieleza kuwa kwa sasa taasisi hiyo inakosa nguvu ya kisheria hata inapobaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria za mazingira.

Kadhalika Mbunge wa Bumbuli, Mhandisi Ramadhan Hamza Singano, aliongeza kuwa pamoja na NEMC kufanya kaguzi katika sekta mbalimbali ikiwemo migodi, gesi na mafuta, bado inakabiliwa na uhaba wa rasilimali kutokana na mgao mdogo wa bajeti.

Kwa upande wake, Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mhe. Joshua Nassari, aliunga mkono hoja hiyo akitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi kuimarisha NEMC ili iweze kusimamia kikamilifu uhifadhi wa mazingira.

Wabunge hao walisisitiza kuwa bila kuipa NEMC mamlaka kamili na rasilimali za kutosha, jitihada za kulinda mazingira nchini zitabaki kuwa dhaifu.

# MIAKA 40 YA NEMC: SAFARI YA TANZANIA KUELEKEA MUSTAKABALI WA KIJANI NA MAENDELEO ENDELEVU

Katika dunia inayokabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira na kupungua kwa rasilimali asilia, Tanzania inaendelea kuwa mfano wa matumaini na uthabiti kupitia juhudi zake za kulinda mazingira. Maadhimisho ya miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) yalionesha dhamira ya Taifa kulinda mazingira huku likiendeleza uchumi.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1986, NEMC imekuwa mhimili wa usimamizi wa mazingira nchini. Zaidi ya miradi 35,000 imepitia Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA), hatua iliyosaidia kuoanisha maendeleo ya kiuchumi na ulinzi wa mazingira. Pia, utoaji wa vibali zaidi ya 28,000 umeimarisha uzingatiaji wa viwango vya mazingira na kuongeza ushindani wa bidhaa za Tanzania kimataifa, huku juhudi za kudhibiti uchafuzi zikiepusha gharama kubwa za kurekebisha madhara.

Katika kujenga uwezo, wataalamu zaidi ya 12,000 wamepata mafunzo, na hivyo kuimarisha usimamizi wa mazingira katika sekta mbalimbali. Hii inaonesha kuwa mazingira si suala la pembeni bali ni msingi wa uchumi wa taifa, hasa katika sekta kama kilimo na utalii zinazotegemea rasilimali asilia.

Hata hivyo, changamoto bado zipo. Uharibifu wa misitu, kilimo kisicho endelevu na matumizi ya nishati zisizo rafiki vinaendelea kuathiri mazingira. Aidha, athari za mabadiliko ya tabianchi kama ukame na mafuriko zinaathiri maisha ya wananchi na uzalishaji. Hali hii inahitaji si sera pekee bali pia mabadiliko ya mtazamo, matumizi ya teknolojia na ushirikiano wa wadau wote.

Kupitia ushirikiano huo, wananchi zaidi ya milioni 4.2 walifikiwa na elimu ya mazingira, huku sekta binafsi ikiongeza uwekezaji katika teknolojia safi na uzalishaji endelevu. Maboresho ya Sera na Sheria pia yaliweka Tanzania katika nafasi nzuri ya kimataifa katika masuala ya mazingira.

Kuelekea kilele cha maadhimisho tarehe 29 Mei 2026, shughuli kama upandaji wa miti 40,000 na utoaji wa elimu zilionesha dhamira ya kuchukua hatua zaidi. Huu ni wakati wa kutafakari urithi tunaotaka kuacha kwa vizazi vijavyo.

Kwa ujumla, mafanikio ya miaka 40 ya NEMC yalionesha kuwa Tanzania ina uwezo wa kufikia maendeleo endelevu. Hata hivyo, mafanikio ya baadaye yatategemea maamuzi ya sasa, ambapo kila Mtanzania ana wajibu wa kulinda mazingira kwa vitendo.

***#MazingiraYetuUhaiWetu – Tuyatunze, Yatutunze***

*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi akizungumza na vyombo mbalimbali vya habari kuelekea miaka 40 ya NEMC.*



# DG NEMC AELEZA UMUHIMU WA VYOMBO VYA HABARI KWENYE MASUALA YA MAZINGIRA




*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa NEMC*

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa na ya kimkakati katika kulinda, kuhifadhi na kuendeleza mazingira nchini, hasa katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na changamoto kama mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira, ukataji miti hovyo, upotevu wa vyanzo vya maji na ongezeko la taka.

Dkt. Semesi aliyasema hayo Mei 21,2026 alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari za mazingira kwenye kikao cha wadau hao kilicholenga kupokea maoni kuelekea Maadhimisho ya Miaka 40 ya NEMC.

Alisema kupitia redio, televisheni, magazeti, mitandao ya kijamii na majukwaa ya kidijitali, vyombo vya habari vimeendelea kuwa daraja muhimu kati ya Serikali, wataalamu na wananchi katika kujenga uelewa na kuhamasisha hatua za kulinda mazingira.

“Kwanza, vyombo vya habari vina jukumu muhimu la kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa mazingira na madhara ya kuyaharibu. Kupitia habari, vipindi maalum, makala na kampeni mbalimbali, wananchi hupata uelewa kuhusu masuala kama mabadiliko ya tabianchi, usimamizi wa taka, uhifadhi wa vyanzo vya maji, matumizi endelevu ya rasilimali za asili na umuhimu wa upandaji miti” alisema Dkt. Semesi.

“Vyombo vya habari vina nafasi ya kuibua na kufuatilia changamoto za kimazingira, kuhamasisha ushiriki wa jamii katika shughuli za mazingira kama kampeni za usafi, upandaji miti, matumizi ya nishati safi na urejelezaji wa taka. Vyombo vya habari pia ni kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi, katika zama za kidijitali, matumizi ya mitandao ya kijamii na teknolojia kama video fupi, infographics, podcasts na kampeni za mtandaoni yameongeza uwezo wa kufikisha elimu ya mazingira kwa haraka zaidi, hasa kwa vijana ambao ni nguvu kazi muhimu ya taifa” aliongezea Dkt. Semesi.

Aidha, alisisitiza kuwa kwa ujumla vyombo vya habari vina nafasi ya kujenga Taifa lenye utamaduni wa kuthamini na kutunza mazingira, kwa kusisitiza uwajibikaji wa kila mmoja katika kulinda rasilimali za asili kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.



*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Sware Semesi (katikati) akiwa na baadhi ya Viongozi wa NEMC pamoja na Wahariri na Waandishi wa Habari katika Ofisi za NEMC, Mikocheni Jijini Dar es Salaam.*

# NEMC NA TORONTO METROPOLITAN UNIVERSITY (TMU) YA NCHINI CANADA ZAKUTANA KUJADILI CHANGAMOTO ZA KIMAZINGIRA



*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Sware Semesi, (kulia) akiwa na Bi Angela Murphy wa Toronto Metropolitan University kujadili changamoto zinazoibuka za ubora wa maji ikiwemo microplastics, PFAS ("forever chemicals")*

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Sware Semesi alikutana na Bi. Angela Murphy wa Toronto Metropolitan University kujadili changamoto zinazoibuka za ubora wa maji ikiwemo microplastics, PFAS ("forever chemicals"), kemikali za sintetiki zisizodhibitiwa na uchafuzi wa kloridi unaotokana na chumvi za barabarani.

Majadiliano hayo yalisisitiza umuhimu wa kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa vichafuzi hivyo kwa ajili ya kulinda mazingira na afya ya jamii. Ambapo pia Dkt. Semesi alipata fursa ya kujifunza kuhusu tafiti zinazoendelea za matumizi ya microplastics zenye alama za DNA kufuatilia mwenendo wa vichafuzi katika mazingira ya maji.

Majadiliano hayo pia yalifungua fursa za ushirikiano wa kitaaluma na kitaasisi kati ya Canada na Tanzania katika usimamizi wa ubora wa maji na mazingira.



*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Sware Semesi, (kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja wa wenyeji wake baada ya majadiliano katika Mji wa Toronto.*

Ziara hii kupitia Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi iliwezesha NEMC kujifunza zaidi kuhusu kazi za kitaaluma na za kimkakati zinazofanywa na Urban Water TMU katika kukabiliana na changamoto za uchafuzi wa maji mijini. Wakati huo huo pande hizo mbili ziliainisha fursa za ushirikiano kati ya taasisi za utafiti na wadau wa Canada na Tanzania katika masuala ya usimamizi wa mazingira na ubora wa maji.

**#NEMC #WaterQuality #EnvironmentalProtection**

# NEMC YAUNGANA NA WATANZANIA WOTE KUSHEREHEKEA MEI MOSI




*Maafisa kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) waliungana na Watanzania wote kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ngazi ya Mkoa yaliyofanyika Mei 1, 2026 katika viwanja vya Mnazi Mmoja,.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliungana na Watanzania wote kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ngazi ya Mkoa yaliyofanyika Mei 1, 2026 katika viwanja vya Mnazi Mmoja, ambapo Kitaifa yalifanyikia Mkoani Njombe

Akizungumza katika maadhimisho hayo yenye kaulimbiu **"Kazi zenye staha ni nguzo imara kwa maendeleo endelevu katika utekelezaji wa Dira ya 2050"** Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Albert Chalamila alisisitiza umuhimu wa uwajibikaji, nidhamu kazini na uzalendo miongoni mwa wafanyakazi, akieleza kuwa mafanikio ya maendeleo ya mkoa na Taifa kwa ujumla yanategemea juhudi za kila mfanyakazi.

Aidha, alihimiza waajiri kuhakikisha wanaboresha mazingira ya kazi na kuwapatia wafanyakazi nyenzo stahiki ili kuongeza ufanisi na tija.

Kupitia risala ya vyama vya wafanyakazi, ilielezwa kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kupigania ajira zenye staha kwa wote ili kuwawezesha wananchi kuishi maisha bora ikiwemo kulindwa kwa haki za wafanyakazi, kuboreshwa kwa maslahi yao pamoja na kuhakikisha mazingira salama ya kazi yanazingatiwa wakati wote.

Maadhimisho hayo yalikuwa fursa muhimu kwa wafanyakazi na waajiri kutafakari mchango wao katika maendeleo ya taasisi na Taifa, huku kaulimbiu ya mwaka huu ikisisitiza umuhimu wa kazi zenye staha, ulinzi wa haki za wafanyakazi na utekelezaji wa sheria za kazi kama msingi wa maendeleo endelevu.



*Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mhe. Albert Chalamila akihutubia wakati wa maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani yaliyofanyika viwanja vya Mnazi mmoja Jijini Dar es Salaam.*

# BENKI YADUNIA YARIDHISHWA NA UTENDAJI WA NEMC

## Yajipanga kushirikiana katika kuijenga Kimamlaka.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilikutana na ujumbe wa Benki ya Dunia ulioongozwa na Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Bi Anna Wellenstein pamoja na Bw. Muhammad Kandeel, kwa lengo la kujadili namna ya kuimarisha ushirikiano katika kuboresha mifumo ya usimamizi wa mazingira nchini.

Majadiliano hayo yalijikita katika maeneo mbalimbali ikiwemo kuimarisha utekelezaji wa tathmini za athari kwa mazingira, kujenga uwezo wa wataalamu wa mazingira na maafisa wa serikali, pamoja na kuwawezesha wadau mbalimbali kuelewa na kutumia kwa ufanisi mifumo na taratibu za Benki ya Dunia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Timu ya NEMC iliongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Immaculata Semesi.

Katika kikao hicho, NEMC ilitoa shukrani kwa Benki ya Dunia kwa ushirikiano wake mkubwa katika utekelezaji wa Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo (EHPMP), ambao umeleta mafanikio makubwa katika kuimarisha usimamizi wa kemikali na kupunguza athari za zebaki katika shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu nchini. Kwa upande wake, Benki ya Dunia ilieleza kuridhishwa na matokeo ya mradi huo na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa karibu katika kufuatilia na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kupitia mradi huo.



*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Sware Semesi akiwa katika katika picha ya pamoja na ujumbe wa Benki ya Dunia ulioongozwa na Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Bi Anna Wellenstein pamoja na Bw. Muhammad Kandeel*

# MWENYEKITI WA BODI YA NEMC AKIMBIA KILOMITA 5



*Pichani ni Mkurugenzi wa Idara ya Tafiti za Mazingira (NEMC), Dkt. Menan Jangu akisaini mkataba wa Mashirikiano.*

Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mhandisi Mwanasha Tumbo, ameshiriki mbio za kilomita 5 zilizofanyika katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Mbio hizo zililenga kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kuendeleza afya kupitia shughuli za michezo.

Tukio hilo liliwakutanisha viongozi wa Serikali, wadau wa mazingira na wananchi mbalimbali, likibeba ujumbe wa pamoja wa kulinda mazingira kwa maendeleo endelevu na ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo.

# TAKA SI UCHAFU TENA: TANZANIA YAELEKEA UCHUMI WA KIJANI KUPITIA UREJELEZAJI




*Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Baraka Haran Luvanda akizungumza na viongozi wa Serikali, wadau wa mazingira, waokota taka rejeshi, waokota chuma chakavu, sekta binafsi pamoja na wadau wa maendeleokatika mazingira*

Katika hatua muhimu ya kuimarisha usimamizi wa mazingira na kukuza uchumi wa kijani nchini, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lilikutana na wadau wa usimamizi wa taka na urejelezaji jijini Dar es Salaam kujadili mustakabali wa sekta hiyo na nafasi yake katika maendeleo endelevu ya Taifa.

Kikao hicho kilichofanyika Mei 13, 2026 ukumbi wa NEMC, Mikocheni, kiliwakutanisha viongozi wa Serikali, wadau wa mazingira, waokota taka rejeshi, waokota chuma chakavu, sekta binafsi pamoja na wadau wa maendeleo kwa lengo la kujenga mfumo jumuishi wa usimamizi wa taka unaolinda mazingira na kuongeza thamani ya kiuchumi kupitia urejelezaji.

Akifungua kikao hicho, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Baraka Haran Luvanda alisema kuwa Tanzania kwa sasa huzalisha zaidi ya tani milioni 14.4 za taka ngumu kila mwaka, huku karibu nusu ya taka hizo zikizalishwa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Mbeya na Tanga. Alieleza kuwa iwapo taka hizo hazitasimamiwa vizuri zinaweza kusababisha madhara makubwa ikiwemo uchafuzi wa mazingira, magonjwa ya mlipuko, kuziba mifereji na mafuriko.

Hata hivyo, Serikali ilibainisha kuwa taka si tatizo pekee bali pia ni rasilimali yenye uwezo mkubwa wa kuchangia uchumi wa Taifa kupitia dhana ya uchumi mzunguko (Circular Economy). Kupitia mfumo wa "Punguza, Tumia Tena na Rejeleza" maarufu kama 3Rs, Serikali ililenga kubadili mtazamo wa jamii ili kuona taka kama chanzo cha ajira, malighafi na maendeleo.

Katika hotuba yake, Balozi Luvanda aliwatambua waokota taka rejeshi na waokota chuma chakavu kama mashujaa wa kimya wanaochangia kwa kiwango kikubwa kupunguza taka zinazopelekwa dampo, kuongeza viwango vya urejelezaji na kusaidia kupunguza uzalishaji wa gesijoto. Alisisitiza kuwa kazi yao imekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha uchumi wa kijani nchini.

"Waokota taka na waokota chuma chakavu ni sehemu muhimu ya mfumo wa usimamizi wa taka nchini. Kupitia kazi yao, maelfu ya vijana na wanawake wamepata ajira na kipato huku mazingira yakihifadhiwa," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Dkt. Immaculate Sware Semesi, alisema kuwa maadhimisho ya miaka 40 ya NEMC yenye kauli mbiu "NEMC@40: Tunza Mazingira, Linda Taifa" yanapaswa kuwa chachu ya kuongeza uwekezaji na ubunifu katika sekta ya usimamizi wa taka.

Aliyataja makundi kama Tanzania Waste Pickers Association (TAWAPA), Tanzania Recyclers Association(TARA) pamoja na Mtandao wa Waokota Taka Rejeshi Dar es Salaam (MTAWADA) kuwa miongoni mwa wadau muhimu wanaosaidia kusukuma mbele agenda ya uchumi mzunguko nchini.

Dkt. Semesi alibainisha kuwa NEMC imeendelea kushuhudia ongezeko la wawekezaji na taasisi zinazojihusisha na shughuli za ukusanyaji, usafirishaji, uchakataji na urejelezaji wa taka, hali inayodhihirisha kuongezeka kwa mwamko wa uzingatiaji wa sheria za mazingira pamoja na kukua kwa sekta ya uchumi mzunguko nchini.

Aidha, alieleza kuwa matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa taka, ikiwemo mifumo ya kidijitali ya ufuatiliaji wa taka, mashine za uchakataji pamoja na teknolojia za kuzalisha nishati kutokana na taka, yanafungua ukurasa mpya wa uwekezaji na ubunifu nchini Tanzania.



*Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Baraka Haran Luvanda katikati, kulia kwake ni mkurugenzi mkuu wa NEMC*



*Mdau wa mazingira akitoa maoni katika kikao cha wadau*

# SERIKALI YASISITIZA UWAJIBIKAJI WA MAZINGIRA KWA VIWANDA NA WADAU WA TAKA HATARISHI

Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa kuzingatia Sheria za mazingira kwa sekta ya viwanda, kampuni za uteketezaji taka pamoja na wadau wanaohusika na uhifadhi wa bidhaa hatarishi, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kulinda afya za wananchi na kuhakikisha maendeleo endelevu ya Taifa.

Hayo yalijadiliwa katika mkutano wa wadau wa mazingira ulioandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), uliowakutanisha wamiliki wa viwanda, wateketezaji wa taka na wenye maghala ya bidhaa hatarishi kwa lengo la kujadili namna bora ya kuimarisha usimamizi wa mazingira nchini.

Akizungumza katika kikao hicho, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Reuben Kwagila, alisema ukuaji wa sekta ya viwanda unapaswa kwenda sambamba na utekelezaji wa sheria za mazingira ili kupunguza athari zinazoweza kuhatarisha afya za wananchi na mazingira.

Alieleza kuwa mazingira ni msingi muhimu wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, hivyo kila mdau wa uzalishaji na usimamizi wa taka ana wajibu wa kuhakikisha shughuli zake zinafanyika kwa kuzingatia viwango vya usalama wa mazingira na afya.

Katika kikao hicho, Serikali ilisisitiza umuhimu wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ikiwemo udhibiti wa uchafuzi wa hewa, maji na ardhi unaotokana na shughuli za viwanda pamoja na usimamizi sahihi wa taka ngumu na taka hatarishi.

Aidha, wadau walikumbushwa umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kabla ya kuanza miradi ya maendeleo pamoja na kufanya ukaguzi wa mazingira mara kwa mara ili kuhakikisha shughuli za uzalishaji zinaendana na matakwa ya sheria.

Mkutano huo pia uliangazia changamoto zinazotokana na ongezeko la taka za viwandani na matumizi ya kemikali hatarishi, ambapo NEMC ilihimiza matumizi ya teknolojia safi na mifumo bora ya uteketezaji na urejelezaji taka ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Katika kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali, Serikali iliendelea kuhamasisha utekelezaji wa dhana ya Uchumi Mzunguko (Circular Economy) inayolenga kupunguza uzalishaji wa taka, kutumia tena bidhaa na kurejeleza malighafi kwa matumizi mengine ya kiuchumi.

Wadau wa mazingira walielezwa kuwa utekelezaji wa mfumo huo unaweza kusaidia viwanda kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali pamoja na kuongeza ushindani wa bidhaa katika soko la ndani na kimataifa.

Kwa upande wake, NEMC ilisisitiza kuwa ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi na wataalam wa mazingira ni muhimu katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na sekta ya viwanda inayozingatia sheria, inalinda mazingira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

Mkutano huo ulitajwa kuwa jukwaa muhimu la kubadilishana uzoefu, kujadili changamoto zinazokabili wadau wa mazingira pamoja na kuibua mapendekezo yatakayosaidia kuboresha utekelezaji wa sheria za mazingira nchini.

Kupitia mikutano kama hiyo, Serikali inalenga kujenga uelewa mkubwa kwa wadau kuhusu umuhimu wa matumizi salama ya kemikali, uhifadhi sahihi wa bidhaa hatarishi, usimamizi wa taka na uwekezaji katika teknolojia rafiki kwa mazingira kwa ajili ya ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho.




*Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa akizungumza katika mkutano wa wadau wa mazingira ulioandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)*



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Reuben Kwagilwa (Katikati) akiwa na Mkurugenzi Mkuu -NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi , (kushoto) na Mkurugenzi wa utekelezaji na uzingatiaji wa sharia NEMC, Ndugu Elbariki Bajuta (kulia) katika picha pamoja na wadau wa Mazingira mara baada ya kukamilika kikao cha wadau*

# NEMC KANDA YA ILALA, HALMASHAURI NA WADAU WA MAZINGIRA WASAFISHA FUKWE ZA DARAJA LA SALENDER



*Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo,(kushoto) akiwa na Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC), Bw. Elibariki Bajuta (kulia) katika zoezi la usafi daraja la Selander*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ilala kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, JUZA, Care and Help, Chuo cha Maji, MUHAS pamoja na wadau wa mazingira walifanya zoezi la usafi katika fukwe za Daraja la Salender zilizopo Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam. Zoezi hilo lilihusisha ukusanyaji wa taka zilizokuwa zimetapakaa katika maeneo ya fukwe kwa lengo la kulinda mazingira na afya za wananchi.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC), Bw. Elibariki Bajuta alisema ushirikiano kati ya taasisi na wananchi katika shughuli za usafi wa mazingira ni muhimu katika kuhakikisha maeneo ya pwani na vyanzo vya maji vinaendelea kuwa salama na endelevu.

"Uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu, hivyo tunapaswa kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za usafi na utunzaji wa mazingira," alisema Bajuta.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mhe. Edward Mpogolo alilipongeza juhudi za NEMC na wadau walioshiriki katika zoezi hilo huku akisisitiza umuhimu wa wananchi kuacha tabia ya kutupa taka ovyo katika maeneo ya fukwe na mifereji ya maji.

"Tunapaswa kujenga utamaduni wa kutunza mazingira yetu kila siku ili kuyaacha salama kwa vizazi vijavyo," amesema Mhe. Mpogolo.

Zoezi hilo lilikuwa sehemu ya juhudi zinazoendelea za kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa usafi wa mazingira, uhifadhi wa maeneo ya pwani pamoja na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaoweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu na viumbe hai wa baharini.

# NEMC YATAMBUA SHULE BORA ZA UHIFADHI WA MAZINGIRA DAR ES SALAAM

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitoa tuzo na vyeti kwa shule za Msingi zilizofanya vizuri katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Kimkoa Juni 5, 2026 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, yakiongozwa na kauli mbiu isemayo, "Dira 2050: Tuwajibike Kukijanisha Tanzania.

Akizungumza katika Kilele cha Maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mhe. Edward Mpogolo, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira ili kuhakikisha Tanzania inakuwa salama na endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Alisema utunzaji wa mazingira ni msingi muhimu wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, huku akisisitiza umuhimu wa kuwajengea vijana na wanafunzi utamaduni wa kulinda mazingira tangu wakiwa wadogo.

"Tunahitaji kuongeza juhudi za pamoja katika kulinda mazingira yetu, kwani mafanikio ya Dira 2050 yanategemea namna tunavyohifadhi rasilimali za mazingira na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi," amesema Mhe. Mpogolo.

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Kaimu Meneja wa Kanda ya Ilala, Bi. Zainab Kuhanwa, alisema kuwa NEMC kwa kushirikiana na KPMG Advisory Limited iliandaa mashindano maalum kwa shule za msingi za Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kutambua na kuthamini juhudi zilizofanywa na shule hizo katika kuhifadhi mazingira na kujenga kizazi chenye mwamko wa kulinda rasilimali za asili.

Alieleza kuwa mchakato wa kupata washindi ulifanywa na timu ya wataalamu kutoka NEMC na KPMG kwa kuzingatia vigezo ikiwemo uwepo wa klabu hai za mazingira, walimu wa mazingira, upandaji na utunzaji wa miti, bustani za maua, usimamizi na utenganishaji wa taka, maeneo ya kuhifadhi taka, mabango ya elimu ya mazingira pamoja na usafi wa vyoo.

Bi. Kuhanwa alibainisha kuwa utoaji wa tuzo na vyeti hivyo kwa shule kumi bora ni sehemu ya jitihada za kuhamasisha wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla kuendeleza utamaduni wa kuhifadhi mazingira. Alisema hatua hiyo inalenga kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuwa mabalozi wa mazingira katika jamii zao na kuhamasisha wadau wengine kuiga mifano bora ya usimamizi wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Taifa.



# WAZIRI MASAUNI ASITISHA SHUGHULI ZA KIWANDA CHA AFRICAN STEEL KWA UCHAFUZI WA MAZINGIRA



*Shehena ya vifungashio na vibebeo vilivyokamatwa kwenye operesheni maalumu ya kutokomeza mifuko ya Plastiki nchini kabla ya kuteketezwa katika Kiwanda cha Dangote mkoani Mtwara.*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Hamad Masauni, alisitisha shughuli za kiwanda cha African Steel Group Company Limited kilichopo Kijiji cha Mwavi, Kata ya Fukayosi, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, kinachotumia chuma chakavu kuzalisha nondo kwa ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za uhifadhi wa mazingira.

Hatua hiyo ilifikiwa wakati wa ziara ya Waziri Masauni ya kukagua utekelezaji wa Sheria za mazingira katika viwanda vitatu vilivyopo Wilaya ya Bagamoyo, ambapo amekipongeza kiwanda cha KAMAL Refinery Limited kinachojishughulisha na uchakataji wa mafuta machafu na Roster Vehicle Equipment Limited kinachojihusisha na utengenezaji na uunganishaji wa magari (truck assembly) kwa Usimamizi mzuri wa Sheria ya Mazingira

Akizungumza wakati wa ukaguzi huo, Waziri Masauni alisema Kiwanda cha African Steel kimeendelea kuchafua mazingira licha ya kupewa maelekezo mara kadhaa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kufuatia ukaguzi uliofanyika lakini kimepuuza na kushindwa kuyatekeleza, hali iliyoilazimu Serikali kuchukua hatua ya kusitisha shughuli zake.

Alitaja ukiukwaji uliobainika kuwa ni uchafuzi mkubwa wa hewa unaotokana na moshi mzito unaohatarisha afya za wafanyakazi na wananchi, utiririshaji wa majitaka kwenye mazingira, utupaji holela wa taka pamoja na kukosekana kwa eneo maalumu la kuhifadhi chuma chakavu, hali inayosababisha uchafuzi wa ardhi. Kutokana na hali hiyo, ameamuru shughuli za kiwanda hicho kusitishwa hadi kitakapotekeleza kikamilifu maelekezo ya NEMC na Serikali.

Aidha, Waziri Masauni aliipongeza NEMC kwa kazi kubwa ya ukaguzi na usimamizi wa mazingira nchini, huku Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Dkt. Immaculate Sware Semesi aliahidi kuendelea kusimamia kikamilifu Sheria ya Mazingira katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuhakikisha viwanda vinazingatia matakwa ya kisheria.

Waziri Masauni alisisitiza kuwa lengo la Serikali si kusitisha uwekezaji, bali kuhakikisha shughuli zote za uzalishaji zinafanyika kwa kuzingatia sheria, kulinda afya za wananchi na kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu.

# NEMC YASHIRIKI KONGAMANO LA VIJANA KUJADILI USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA NA DIRA 2050

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliungana na wadau wa Mazingira kushiriki Kongamano la Vijana lililofanyika Juni 2, 2026 katika Ukumbi wa Maktaba wa chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), likiwa na kaulimbiu isemayo "Ushiriki wa Vijana katika Kutekeleza Dira 2050: Usimamizi Endelevu wa Mazingira na Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi."




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni akizungumza katika kongamano la vijana kuelekea siku ya mazingira duniani

Akifungua kongamano hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, alisisitiza umuhimu wa vijana kushiriki kikamilifu katika uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha maendeleo endelevu na utekelezaji wenye mafanikio wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Kupitia kongamano hilo, NEMC ilipata fursa ya kutoa elimu ya mazingira kwa vijana, kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali na kujadili nafasi ya vijana katika kuibua suluhisho bunifu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo ya Taifa ya sasa na vizazi vijavyo.



Baadhi ya washriki kwenye kongamoano la vijana, pamoja na baadhi ya watumishi wa NEMC

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA ROBO MWAKA ZA NEMC KANDA YA MASHARIKI KUSINI (EZS)



*Maafisa wa NEMC Kanda ya Mashariki kusini wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Kazole Maarifa iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga walipotembelea Shule hiyo katika kwa ajili ya zoezi la upandaji miti.*

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2025/2026, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Kanda ya Mashariki Kusini (EZS) liliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mafanikio makubwa katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Kupitia ukaguzi wa miradi, usimamizi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), utoaji wa elimu kwa umma, upandaji miti na utatuzi wa malalamiko ya kimazingira, Kanda imeendelea kuchangia ulinzi wa mazingira na ustawi wa jamii.

Katika kipindi hicho, Kanda ilifanya kaguzi 87 za miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kanuni zake. Kaguzi hizo ziliwezesha kubaini changamoto za kimazingira mapema na kutoa maelekezo ya kitaalamu kwa wawekezaji na watekelezaji wa miradi ili kuzuia au kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kwa mazingira na jamii.

Sambamba na hilo, Kanda ilipokea na kushughulikia malalamiko 14 ya kimazingira yaliyohusu kelele, uchafuzi wa maji, hewa na usimamizi wa taka. Kupitia uchunguzi na hatua stahiki zilizochukuliwa, malalamiko mengi yalitatuliwa kwa wakati, hivyo kulinda afya ya wananchi na mazingira.

Katika kutekeleza masharti ya Kifungu cha 81 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Kanda iliendelea kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Ukaguzi wa Mazingira. Katika kipindi hicho, ilifanya upembuzi wa miradi 41, ukaguzi wa mazingira wa miradi 26, iliendesha vikao 17 vya tathmini, ilitoa maoni ya kitaalamu (comments) 15, iliwasilisha miradi 20 katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa hatua zaidi za maamuzi, na kufanikisha kutolewa kwa vyeti 23 vya mazingira.

Kuhusu utoaji wa elimu kwa umma, Kanda iliendesha vipindi saba vya redio na vipindi viwili vya televisheni, vikitoa elimu kuhusu usimamizi bora wa taka, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, uhifadhi wa vyanzo vya maji, upandaji miti na wajibu wa wananchi katika kulinda mazingira.

Katika kuimarisha uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Kanda iliratibu na kushiriki upandaji wa miti 3,400 katika wilaya za Kigamboni, Mkuranga, Kibiti, Mafia na Kisarawe. Zoezi hilo lilihusisha ushirikiano kati ya taasisi za umma, sekta binafsi na wananchi, na limechangia kuongeza uoto wa asili pamoja na kuimarisha utamaduni wa utunzaji wa mazingira.

Aidha, Kanda ilishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani katika ngazi za wilaya na mkoa. Katika Wilaya ya Kibiti, ilitoa elimu ya mazingira kwa wanafunzi wa shule za msingi, huku katika ngazi ya mkoa ikishirikiana na kampuni ya KPMG kutambua na kuzawadia klabu za mazingira zilizofanya vizuri katika shule za msingi. Hatua hiyo imelenga kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi katika shughuli za uhifadhi wa mazingira na kujenga kizazi chenye utamaduni wa kutunza mazingira.

Mafanikio haya yanaonesha dhamira ya NEMC Kanda ya Mashariki Kusini katika kuimarisha usimamizi wa mazingira, kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu wajibu wao wa kulinda mazingira na kuendeleza ushirikiano na wadau mbalimbali. Kupitia juhudi hizi, Kanda inaendelea kutoa mchango muhimu katika kufanikisha maendeleo endelevu na kuhakikisha mazingira salama kwa kizazi cha sasa na kijacho.

# NEMC KANDA YA ILALA YAENDELEA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA ZUIO LA MIFUKO YA PLASTIKI JNIA

NEMC Kanda ya Ilala imeendelea kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa zuio la matumizi ya mifuko ya plastiki katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), ambapo timu ya maafisa wake ilianza kazi rasmi tarehe 2 Machi 2026 kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira (Kanuni za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki na Lakili za Chupa za Mwaka 2022). Timu hiyo inaundwa na maafisa Kwilasa Lushanga, Grace Tupa, Mike Obed na Magdalena Kosana, ambao wamekuwa wakiratibu utekelezaji wa sheria hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa uwanja wa ndege.

Katika kutekeleza majukumu yao, maafisa hao wamekuwa wakitoa elimu kwa wafanyakazi wa JNIA, abiria na mashirika ya ndege kuhusu marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki, wakitumia vipeperushi pamoja na mifuko mbadala kama nyenzo za uelimishaji. Hadi sasa, takribani kilo 1,000 za mifuko ya plastiki zimekusanywa kwa ajili ya uteketezaji au urejeleshaji, huku zaidi ya mifuko mbadala 2,000 na vipeperushi zaidi ya 200 vikigawiwa kwa abiria ili kuongeza uelewa wa sheria hiyo.


Mbali na utoaji wa elimu, timu hiyo imekuwa ikishiriki katika vikao vya kila wiki vya wadau wa JNIA vinavyolenga kutathmini utekelezaji wa majukumu na kujadili changamoto zinazojitokeza. Vilevile, maafisa hao wamekuwa wakihudhuria mafunzo mbalimbali yanayoandaliwa na mamlaka ya uwanja wa ndege kwa lengo la kuimarisha uwezo wao na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana, timu imeeleza kuwa changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu wa chumba cha ofisi kwa ajili ya shughuli za kiofisi na kuhifadhi vitendea kazi pamoja na nyaraka za Serikali. Kutokana na hali hiyo, imependekezwa kuwa ofisi itolewe kwa wakati ili kuwezesha maafisa hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kuhakikisha usalama wa nyaraka na vifaa vinavyotumika katika zoezi hilo.




*Afisa Ustawi wa Jamii, Kanda ya Ilala akimkabidhi mfuko mbadala mmoja wapo wa wasafiri katika jengo la Kiwanja cha ndege cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.*

## TAKWIMU HIZI NI KWA ROBO YA NNE, 2025/2026




*Wasiliana nasi;*
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**
Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 713 608 930 Namba ya Bure: 0800 110 115
Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz

**NEMC@40 #TunzaMazingiraLindaTaifa**

+255 680 400 400
@nemctanzania
NemcTVTanzania
www.nemc.or.tz